

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA HAMSINI NA TATU**

**17 JUNI, 2021**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA TATU – TAREHE 17 JUNI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

III. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

440. MHESHIMIWA IDDI KASSIM IDDI  
(MSALALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaipandisha hadhi Halmashauri ya Msalala kuwa Wilaya.

441. MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA  
(KILINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga Daraja linalounganisha Wilaya ya Kilindi na Kiteto kupitia Kijiji cha Sambu.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**442. MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Barabara ya kutoka Kibaoni – Kasansa – Muze – Ilemba – Kilyamatundu hadi Mlowo itajengwa kwa kiwango cha lami.

**443. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini ukarabati na upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Musoma utakamilika.

**WIZARA YA MAJI:**

**444. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itafikisha huduma ya Maji kwa Wananchi wa Kata za Kipatimu, Kibata, Chumo, Kandawale, Namayuni, Miguruwe, Njinjo, Mitole na Kinjimbi katika Jimbo la Kilwa Kaskazini ili kuwaondolea adha ya maji inayowakabili.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

##### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali Kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.



Kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA**  
**17 JUNI, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***  
**KATIBU WA BUNGE**